

Mahusiano Salama

Mada Muhimu

- Uhushiano salama una mawasiliano ya wazi na salama.
- Ridhaa ni makubaliano ya kufanya jambo.
- Mwambie mtu unayemwamini na polisi ikiwa mtu uliye naye ana vurugu au anakufanya uogope.

Uhushiano salama ni upi?

Uhushiano salama una mawasiliano ya wazi na salama. Hauna unyanyasaji wa kimwili na akili. Katika uhushiano usio salama, mtu hufanya uhisi kuogopa na kulazimishwa kufanya kitu.

Ridhaa

Ridhaa ni makubaliano ya kufanya jambo. Hupaswi kuhisi kulazimishwa ili utoe ridhaa. Unaweza kubatilisha ridhaa wakati wowote. Sio salama ikiwa mtu anakulazimisha kufanya kitu baada ya kusema "La" au hukuweza kusema "La". Vitendo vingine visivyo salama ni kulazimishwa kushiriki ngono na kuguswa au kupigwa busu bila kutaka.

Usalama wa Kimwili na Akili

Wewe huwa salama kimwili wakati huogopi kuwa kuguswa kutakuwa kwenye vurugu au kusikohitajika. Huenda usiwe salama kimwili ikiwa mtu anakugonga, anakupiga makofi, ngumi, mateke, anavuta nywele zako, anakusukuma, anakuuma, anakunyonga au anatumia silaha kwako.

Akili yako ni salama wakati uko huru kutoptana na matusi au unyanyasaji wa kihisia. Unyanyasaji unaweza kuwa wakati mtu anasema au anafanya kitu kinachokufanya uhisi hofu au uhisi vibaya kujihusu. Huenda usiwe salama ikiwa mtu anakunyanya, anakupigia makelele na anakutusi. Aina zingine za unyanyasaji zinaweza kuwa wakati mtu anakuambia unachoweza au usichoweza kufanya, au mtu anatishia kukuumiza wewe au kujiumiza.

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara:

Je, ninapaswa kupigia simu polisi?

Ndiyo. Vurugu za nyumbani ni uhalifu. Polisi wanaweza kukupeleka wewe na watoto wako kwenye nyumba ya familiaau rafiki yako au mahali salama kama makazi ya wanawake. Ikiwa afisa wa polisi hazungumzi lugha yako, tafuta mtu ambaye sio mtoto wako, mume wako au mpenzi wako ili afanye ukalimani. Kila wakati muulize afisa wa polisi ajaze "ripoti ya tukio," ambayo inaelezea kile kilichotokea.

Je, ninaweza kupata amri ya ulinzi hata kama mimi sio Raia wa Marekani?

Ndiyo. Huhitaji kuwa raia au mkazi wa kudumu kisheria ili upate amri ya ulinzi.

Unaweza kupata fomu ya maombi katika mahakama, makao ya wanawake, ofisi za huduma za kisheria na idara zingine za polisi.

Mume wangu anatishia kuchukua watoto wangu ikiwa nitamwacha. Ninaweza kufanya nini?

Ikiwa mume wako au mpenzi wako anatishia kuchukua watoto wako au kwenda nao katika nchi yake ya nyumbani, pata usaidizi kwa kutumia hatua zifuatazo:

These materials have been approved by the Minnesota Center of Excellence in Newcomer Health.

Thank you to the Colorado Department of Human Services for donating this material for adaptation and translation.



1. Pata "amri ya ulezi." Amri inaweza kumzua mumeo au rafiki yako wa kiume asichukue watoto kutoka Marekani.
2. Tuma nakala ya amri ya ulezi kwa Idara ya Idara ya Sera za Nje ya Nchi ili kumzua kupata visa au pasipoti za watoto. Tuma nakala kwa ubalozi nchini Marekani wa nchi ya nyumbani ya mumeo au mpenzi wako.
3. Peana nakala ya amri hiyo katika shule za watoto. Waambie wafanyakazi wa shule wasipeane watoto kwa yejote isipokuwa wewe.

Je, nitahamishwa ikiwa nitachukua hatua yoyote kati ya hizi?

Hapana. Huwezi kuhamishwa ikiwa utaripoti mtu kwa vurugu za nyumbani.

These materials have been approved by the Minnesota Center of Excellence in Newcomer Health.
Thank you to the Colorado Department of Human Services for donating this material for adaptation and translation.

